# Yesu na Maria Magdalena: Walikuwa na ndoa ya siri?

## Misezi Yesu

Je, historia imekuwa sio sahihi kwa miaka 2000—kulikuwa na Mrs. Yesu Kristo? In, "*Kaburi la Familia ya Yesu*," mkurugenzi wa (makala ya Chaneli ya TV ya *Discovery*) Simcha Jacobovici anadai kuna "ushahidi" kwamba Yesu na Maria Magdalena walioana na walikuwa na mtoto aliyeitwa Yuda.

(Kuona kitu gani wasomi wanasema kuhusu "ushahidi" wa Jacobovici angalia, saa Wasifu Uliozaliwa.)

Jacobovici si mtu wa kwanza kudai uhusiano wa kimapenzi unaowezekana kati ya Yesu na Maria . Sinema, *Jaribio la Mwisho la Kristo*, na vitabu kama *Damu Takatifu, Kikombe Kitakatifu, na maandishi ya Da Vinci*, yalifanya siri uhusiano kati ya Yesu na Maria kuwa sehemu kuu ya habari zao.

*Maandishi ya Da Vinci* yanaanza na ukurasa wa ukweli ambao unafanya hadithi ya kutunga kuonekana kuwa kweli katika madai yake yote. Kitabu kimevunja rekodi zote katika orodha ya mauzo bora ya New York, na imefuatiwa na sinema fanikifu kibiashara. Ukusanya hodari wa ukweli wa mtunzi Dan Brown pamoja na ubunifu umewaaminisha wasomaji wengi kwamba Yesu na Maria Magdalena walikuwa wameoana na walikuwa na mtoto (Angalia saa Tabasamu la MonaLisa). Lakini madai haya ya kimapenzi yanatangaza sana vitabu na sinema, au yanaungwa mkono na ushahidi wa kihistoria.

## Maria wa Siri

Kabla hatujachunguza ushahidi kwa mapenzi yoyote yanayowezekana kati ya Yesu na Maria Magdalena, tuangalie mtu huyu Maria kutoka mji mdogo wa Galilaya wa Magdala. Kwa kuanza tunauliza swali, ni maandiko gani ya kale yanatoa mwanga kwa tabia yake na uhusiano wake na Yesu wa Nazareth?

Injili za Agano Jipya ni rekodi za zamani za Maria wa Magdala. Katika Injili Maria anaelezewa kama mwanamke ambaye Yesu alimponya kumilikiwa na mashetani. Injili (Mathayo, Marko, Luka na Yohana) zinamwelezea Maria kama mfuasi wa Yesu ambaye alisikiliza mafundisho yake, alitoa mahitaji yake ya kifedha, alishuhudia kusulubiwa kwake, na siku tatu baadaye alikuwa wa kwanza kumuona hai.

Baadhi wamesema Maria Magdalena alikuwa malaya, lakini si mitume wala kanisa la kale wamemzungumzia zaidi ya kusema alikuwa mmoja wa wafuasi wa karibu wa Yesu. Wazo kwamba alikuwa malaya lilianza karne ya sita, wakati Papa Gregory wa Kwanza alipomtambua yeye kama mwanamke aliyezungumziwa katika Luka 7:37, na mwanamke aliyeosha miguu ya Yesu kwa nywele zake.

Ingawaje maoni ya Papa yawezekana yalisababishwa na ukweli kwamba Yesu alipunga mapepo saba kutoka kwake, hakuna msomi wa Biblia anaweza kufanya mhusisho kuhusu Mary Magdalena na mwanamke katika vifungu vya Luka. Kwa nyongeza, Injili za Agano Jipya hazidokezi kitu chochote kile cha kimapenzi kati ya Yesu na Maria.

Hivyo wapi wananadharia wa hila wanapata wazo? Kwanini madai haya yote? Kwa hilo tunageukia maandiko yaliyoandikwa miaka 100 – 200 baada ya Injili za Agano Jipya na dhehebu lisilo la kikristu lililoitwa Wanostiki (Wazushi/Wajuaji wachache) (Angalia saa Injili Za Siri) Maandiko haya si sehemu ya Agano Jipya, na yalikataliwa na wakristu wa kale kuwa ni ya kizushi na yako kinyume. Hao wanaoandika uhusiano wa kimapenzi katia ya Yesu na Maria wananukuu vifungu vichache kutoka maandiko mawili ya maandiko hayo, Injili ya Maria na Injili ya Philipo. Tuangalie katika vifungu hivyo.

## Injili ya Maria (Magdalena)

Wazo kwamba Maria Magdalena alikuwa mtu maalum kwa Yesu inachukuliwa hasa kutoka Injili ya Maria. Injili hii ya Kinostiki (Kijuaji) si sehemu ya Agano Jipya, na iliandikwa na mtunzi asiyejulikana katika nusu ya karne ya pili, au karibia miaka mia na hamsini baada ya kifo cha Yesu. Hakuna mashahidi wa macho, akiwamo Maria

mwenyewe wangekuwa hai wakati ilipoandikwa (karibia miaka 150 A. D.). Tarehe hiyo ya mwishoni inamaanisha Injili ya Maria haikuandikwa na shahidi wa macho wa Yesu, na hakuna anayejua aliyeiandika.

Aya moja katika Injili ya Maria inamwelezea Maria Magdalena kama mfuasi kipenzi wa Yesu, inasema alimpenda Maria zaidi kuliko sisi (maana yake wafuasi wake)" Katika aya nyingine Peter inavyoaminika alimwambia Maria, Dada, twajua mwokozi alikupenda zaidi ya mwanamke mwingine yeyote" Lakini hakuna kilichoandikwa katika Injili ya Maria kinachozungumzia mapenzi au uhusiano wa kimapenzi kati ya Maria Magdalena na Yesu.

## Injili ya Philipo

*Maandiko ya Da Vinci* yameweka dai lake kwamba Yesu na Maria walikuwa wameoana na walikuwa na mtoto kwenye aya moja pekee katika Injili ya Kinostiki (Kijuaji) ya Philipo ambayo inaonesha Yesu na Maria walikuwa marafiki. Aya hii inasema: (Mabano yanaonekana ambapo maneno ya andiko yanakosekana au hayasomeki)

> "Wanawake watatu siku zote walitembea na BWANA: Maria mama yake, dada na Maria Magdala ambaye aliitwa mwenzi wake. Kwa "Maria" ni jina la dada yake, mama yake na mwenzi/rafiki wake"

In *mtaalamu wa Maandiko ya kubuni ya Da Vinci,* Sir Leigh Teabing anasema kwamba neno kwa neno rafiki lingeweza kumaanisha mwenzi. Lakini kulingana na wasomi, hiyo ni tafsiri isiyoelekea. Kwa kuanza, neno kwa ujumla lililotumika kwa mke katika Agano Jipya Kigiriki ni "gune" sio "koinonos" Ben Witherington III, akiandika katika Rejea ya Kibiblia ya Elimu-Kale, alizungumzia pointi hii muhimu:

> "Kulikuwa na neno lingine la Kigiriki, gune, ambalo lingeweka neno hili wazi. Ni kama neno koinonos hapa linamaanisha "dada" katika maana ya kiroho kwa sababu hivyo ndivyo linavyotumika mahali pengine pote katika aina hii ya uandishi. Katika hali yoyote, maandishi haya hayasemi waziwazi wala kudokeza kwamba Yesu alikuwa amemuoa Maria Magdalena."[1]

Kuna aya moja pia katika Injili ya Philipo ambayo inasema Yesu alimbusu Maria.

> "Mwenzi ni Maria wa Magdala. Alim… yeye zaidi ya wafuasi, alimbusu yeye mara nyingi kwenye. Mwingine …alimwambia, 'Kwanini unampenda yeye zaidi kuliko sisi sote?'"

Kuwasalimia marafiki kwa busu kulikuwa kawaida katika karne ya kwanza, na hakukuwa na ishara ya mapenzi. Profesa Karen King anaeleza kwenye kitabu chake Injili ya Maria Magdala, kwamba busu katika maandiko ya Philipo hasa ilikuwa ni busu safi lisilo la mapenzi bali la ushirika/umoja.

Lakini labda muhimu zaidi ni ukweli kwamba Injili ya Philipo iliandikwa na mtunzi asiyejulikana karibu miaka 200 baada ya maelezo ya mashahidi wa macho wa Agano Jipya (Angalia saa Andiko la Yesu na saa Tabasamu la MonaLisa.

Ni muhimu pia kufahamu kwamba, mbali ya hivi vifungu vichache kwa kuulizwa, hakuna andiko lingine la kihistoria ambalo linadokeza Yesu na Maria walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Hakuna mwanahistoria wa kawaida, au mwanahistoria wa kikristu aliyeandika hata robo kuhusu uhusiano huo. Na kwa sababu Injili zote, Injili ya Maria na Injili ya Philipo ziliandikwa miaka 100 – 220 baada ya Kristo na watunzi wasiojulikana, maelezo yao kuhusu Yesu na Maria yanahitaji kutathminiwa katika mazingira yote ya historia ya wakati ule na maandiko ya mwanzoni kabisa ya Agano Jipya.

## Uamuzi wa Wasomi

Lakini je, kanisa la kale lingeweza kuharibu ushahidi katika jaribio lao la kuandika upya historia ya Yesu? Bila shaka hicho ndicho kitu Jacobovici, Brown, na kundi la wapiga chuku yaani waandika vioja au wadadisi wengine wanachosema. Lakini wasomi wanakubaliana nacho?

*Makala ya gazeti la Newsweek* inaandika kwa kifupi maoni ya wasomi yanayoongoza, kwa uwazi yakisema kwamba wazo la Yesu na Maria Magdalena walioana hayana msingi wa kihistoria. Labda wanostiki yaani wazushi wajuaji wachache walifikiri Agano Jipya lilikuwa na aibu kuhusiana na mapenzi na wakaamua kulikoleza suala hilo kidogo. Kwa sababu yoyote ile, aya hizi zilizotengwa na zilizojificha ziliandikwa miaka 100 – 200 baada ya Kristo haziko zaidi katika kuikita nadharia ya hila za njama juu yake. Usomaji wa kuvutia labda, lakini kabisa siyo historia.

Lakini baadhi wanabaki hawaamini. Labda wanataka tu kuifanya historia ivutie zaidi. Mwandishi wa habari za televisheni aliyeshinda tuzo Frank Sesno aliuliza jopo la wasomi wa kihistoria kuhusu tabia ya kuvutiwa na kitu watu waliyo nayo kwa nadharia ya hila za njama. Profesa Stanley Kutler kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin alijibu, “Wote tunapenda matukio ya ajabu ya siri, lakini tunapenda habari za njama zaidi.”[3]

Labda habari zote kuhusu Yesu na Maria zina umuhimu zaidi wa kufanya kwa wapinzani wa ukristu wakijaribu kumfanya aonekane binadamu wa kawaida mtu ambaye wakristu tangu mwanzo wamemwita “Mungu” (Kusoma zaidi kuhusu jinsi gani wakristu wa zamani walimwona Yesu (Angalia saa Tabasamu la MonaLisa). Kwa mfano, mtume Paulo alisema kuhusu Yesu Kristo:

“Ingawa alikuwa Mungu, hakuhitaji na kushikilia hadhi zake kama Mungu. Alijifanya hana kitu, alichukua nafasi ya unyenyekevu ya mtumwa na alionekana katika umbo la kibinadamu” (Wafilipi 2:6, 7a).

Yohana, shahidi wa macho, na mmoja wa wafuasi wa karibu wa Yesu, alimzungumzia hivyo.

“Katika mwanzo neno tayari lilikuwapo. Alikuwa pamoja na Mungu, na alikuwa Mungu… aliumba kila kitu kilichopo… hivyo neno likawa mwanadamu na likaishi hapa duniani miongoni mwetu.”(sehemu za Yohana 1:1-3, 14).

## Je ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu?

Swali kubwa kabisa la wakati wetu si kwamba Yesu na Maria Magdalena walioana, lakini “Nani ni Yesu Kristo wa Kweli?” Alikuwa mtu wa kipekee, au alikuwa Mungu katika mwili, kama Paulo, Yohana, na wafuasi wake wengine walivyoamini?

Mashahidi wa macho kwa Yesu Kristo kwa kweli walizungumza na walitenda kama walivyoamini, aliinuka kimwili toka katika wafu baada ya kusulubiwa kwake. Ikiwa hawakuwa sahihi basi Ukristu umejengwa katika uongo. Lakini kama walikuwa sahihi, muujiza huo ungethibitisha yote Yesu alisema kuhusu Mungu, yeye mwenyewe na sisi.

Lakini lazima tuchukue ufufuko wa Yesu Kristo kwa imani pekee, au kuna ushahidi mzito wa kihistoria? Wakosoaji wachache walianza uchunguzi kwenye rekodi za kihistoria kuthibitisha maelezo ya ufufuko ni uongo. Ni kitu gani waligundua? Saa Yesu Alifufuka Wafu.

## Kulikuwa na Hila za Da Vinci ?

“Tabasamu la Monalisa” inachunguza fikra kuhusu njama zinaoongoza duniani kuhusu Yesu Kristo. Je, Yesu na Maria Magdalena waliooana? Je Constantine aliagiza uharibifu wa rekodi za kweli za Yesu Kristo akimwelezea upya kuwa Mungu wakristu wanavyomwabudu leo? Saa Tabasamu la MonaLisa.

## Je, Yesu alisema kitu gani kinatokea baada ya sisi kufa?

Ikiwa ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu, basi lazima ajue kitu gani kipo upande mwingine. Ni kitu gani alisema kuhusu maana ya maisha na siku zetu zijazo? Kuna njia nyingi kwenda kwa Mungu au Yesu alidai kuwa njia pekee? Soma majibu ya kushangaza “Kwanini Yesu?” Saa Kwanini Yesu?

## Je, Yesu anaweza kuleta maana katika maisha?

“Kwanini Yesu? inaangalia suala la kwamba Yesu ni muhimu leo. Je, Yesu anaweza kujibu swali kubwa la maisha: “Mimi ni nani?” “Kwanini niko hapa?” na, “Wapi ninaenda?” Makanisa yaliyokufa na misalaba imewaongoza wengine kuamini kwamba hawezi, na kwamba Yesu ametuacha sisi kuendana na dunia iliyo nje isiyo na udhibiti. Lakini Yesu amefanya madai kuhusu maisha na madhumuni yetu hapa duniani ambayo yanahitaji kuchunguzwa kabla hatujamkataa kama asiyejali na asiye na nguvu. Makala hii inachunguza siri ya kwanini Yesu alikuja duniani. Saa www.Kwanini Yesu?

## Ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu?

Mashahidi wa macho kwa Yesu Kristo kwa kweli walizungumza na walitenda kama walivyoamini, alifufuka toka katika wafu baada ya kusulubiwa kwake. Ikiwa walikosea basi uKristu umeanzishwa kwa uongo? Lakini kama walikuwa sahihi, muujiza huo ungethibitisha yote Yesu aliyosema kuhusu Mungu, kuhusu yeye na kutuhusu sisi.

Lakini ni lazima tuamini ufufuko wa Yesu Kristo kwa imani pekee, au kuna ushahidi wowote wa kihistoria? Wakosoaji kadhaa walianza uchunguzi kwenye kumbukumbu za kihistoria kujaribu kuona kama kweli maelezo ya ufufuko yalikuwa uongo. Kitu gani waligundua?

Kuangalia ushuhuda wa madai makuu yaliyowahi kufanyika ya ufufuko wa Yesu Kristo!

Bonyeza hapa kwa ajili ya kudai zaidi fantastic milele alifanya – ya ufufuo wa Yesu Kristo!